

77. Msalabani pa mwokozi

- 1. Msalabani pa mwokozi, hapo niliomba upozi, akaniokoa mpenzi, mwana wa Mungu.*
- 2. Mwana wa Mungu, mwokozi wangu, akaniokoa mpenzi, mwana wa Mungu*
- 3. Chini ya mti msumbufu, niliomba utakatifu, alinikomboa kwa damu, mwana wa Mungu.*
- 4. Aliniokoa dhambini, ikawa kunikaa ndani, aliponifia mtini, mwana wa Mungu.*
- 5. Damu ya Yesu ya thamani, huniokoa makosani, huniendesha wokovuni, mwana wa Mungu.*
- 6. Hicho kijito cha gharama, leo jivike kwa kuzama, kwake uuone uzima, mwana wa Mungu.*